
# REPOA: Uchumi wa nchi hautakuzwa na gesi pekee

› Na Ashura Kishimba



KWA miaka mingi Watanzania walikuwa wakitumia gesi katika sekta mbalimbali ikiwemo viwandani na majumbani.

Ingawa kipindi cha nyuma wananchi waliokuwa wakitumia gesi kama nishati ya kupikia walikuwa ni watu wachache na walionekana wenye kipato cha juu tofauti na hivi sasa gesi inatumiwa na Watanzania walio wengi hata wenye kipato cha kawaida.

Aidha, gesi hiyo iligundulika kwa kipindi kirefu lakini mwaka 2013 ndiyo ilishamiri zaidi baada ya taratibu za maandalizi ya uchimbaji kuanza kufanyika katika Mkoa wa Mtwara, na Watanzania walio wengi wakaanza kuzungumzia gesi kila kona.

Wananchi wa Mkoa wa Mtwara kunakopatikana gesi hiyo walipiga kelele na kuweka migomo ya hapa na pale kwa serikali wakidai kuwa wangeanza kufikiriwa wao zaidi kwa faida itakayopatikana kutokana na gesi hiyo kwa kuwa inatoka kwenye ardhi yao.

Kubwa walikuwa wakilidai wakazi hao ni kutaka kuwepo kwa kiwanda katika Mkoa wao badala ya gesi hiyo kusafirishwa, kwenda mkoani Dar es Salaam.

Lakini, baada ya mazungumzo ya kina kutoka kwa wadau mbalimbali, serikali na wananchi wenyewe hatimaye gesi hiyo ilianza kuchimbwa na kupitishwa mabomba kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.

Japokuwa matumaini ya walio wengi walidhani kuwa baada tu ya kupatikana na kuanza kuchimbwa kwa gesi hiyo hapa nchini ilidhaniwa sasa mambo yatakuwa mteremko, lakini hali inaonekana ni tofauti kwani limetolewa angalizo kutoka kwa watafiti wa masuala ya uchumi waliotafiti katika sekta ya mafuta na gesi hapa nchini.

Imeelezwa kuwa pato la Taifa linalopatikana kutokana na uchimbaji wa gesi Tanzania ni asilimia sita tu, hivyo serikali na wananchi wametakiwa kupunguza matumaini kwenye sekta hiyo na badala yake inapaswa kuanzisha sekta endelevu itakayokuwa mbadala wa rasilimali ya gesi.

Akitoa mada katika mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusiana na uchambuzi wa masuala ya uchumi na mikataba ya mafuta na gesi, Mkurugenzi wa mipango na utafiti wa REPOA, Dk. Abel Kinyondo, anasema matumaini yaliyopo kwa Watanzania walio wengi, na hata baadhi ya wanasiasa kuhusu kupatikana kwa gesi nchini, ni makubwa ikilinganishwa na uhalisia wenyewe.

"Utafiti unaonyesha kuwa gesi hiyo tutakuwa nayo hapa nchini kwa kipindi cha miaka thelathini tu, hivyo kama nchi haitakuwa makini, sekta ya gesi inaweza kushusha uchumi kwani huchangia kiasi cha asilimi sita tu ya pato la Taifa,"

"Asilimia 66.3 ya Watanzania mpaka sasa bado ni wakulima, hivyo inapaswa kuwa makini na upatikanaji huu wa gesi, tunaitumiaje hii gesi katika kuendeleza na kukuza sekta ya kilimo nchini",alisema Dk. Kinyondo.

"Inatupasa tuangalie nyuma kwanza uwepo wa madini nchini kwetu, hasa madini ya Tanzanite ambayo duniani ndiyo yanapatikana Tanzania pekee yametusaidiaje katika kukuza uchumi wetu. Leo hii akiulizwa Mtanzania amenufaika vipi na madini hayo hawezi kupatikana majibu mazuri,"anasisitiza Dk. Kinyondo.

Dk. Kinyondo anabainisha kuwa kabla ya kanuni kukamilika, sera shirikishi na uwezeshaji wazawa Tanzania LCP ya mwaka 2014, sera ya gesi asilia ya mwaka 2013 na sheria ya usimamizi wa mapato ya gesi asilia ya mwaka 2015, serikali iliweka mkakati wa kuhakikisha wazalishaji na kampuni za ndani zinanufaika kwa asilimia 25 wakati wa uzalishaji.

Anasema kinachoweza kusaidia ni serikali kuongeza kodi na kupunguza ushiriki wa sera shirikishi na uwezashaji wazawa Tanzania, LCP kwa Watanzania ili kuepuka wajanja wachache watakaojinufaisha wakati wa uzalishaji.

Kwa upande wake Mkurugenzi mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari anasema endapo Taifa litakuwa na fikra kuwa gesi ndiyo itakuwa mhimili wa uchumi pekee, nchi itapotea.

"Nchi kama Venezuela, Angola na Nigeria ni nchi ambazo zimeathirika sana kiuchumi kwa sababu zilijisahau kuendeleza sekta nyingine na kujikita zaidi katika mafuta. Sasa hivi wananchi wa Venezuela wanapanga foleni ya kupata mkate,"anasema Dk. Mmari.

Mbali na kuangalia kwa kina upatikanaji wa faida kutokana na gesi hiyo, Dk. Mmari anasema katika suala zima la uingiaji mikataba pamoja na wale wanaochaguliwa kwenda kusimamia utendaji maeneo ya uchimbaji hadi usafirishwaji wa rasilimali hiyo, Watanzania wanapaswa kuwa waadilifu na kujenga uzalendo na nchi yao kwa kuwafichua bila woga watu wanaoibia nchi katika sekta ya madini na gesi.

Dakta Mmari anasema kuwa yapo baadhi ya maeneo kama sekta ya mafuta na gesi, Watanzania wamekuwa wakijikwaza wenyewe kwa kuona mtu au mwekezaji anaibia nchi lakini wanashindwa kutoa taarifa katika vyombo husika, matokeo yake uchumi unadumaa.

"Jambo la kushangaza mtu akiona Mtanzania mwenzake anaiba anamsemea, lakini akiiba mzungu hatoi taarifa, au Mtanzania mwenzake akifanya kazi mahali bila kuiba anaonekana mjinga,"anasema Dk. Mmari huku akionekana kuwa mtu mwenye masikitiko makubwa.

Anabainisha kuwa jamii inapaswa kujenga msingi wa nidhamu, kujituma kwa kuwa na maadili katika kazi ili kuiwezesha nchi kuwa na uchumi imara.

Mkurugenzi huyo wa REPOA, anasema katika suala la uchumbaji wa mafuta na gesi ni vema Watanzania wakashirikishwa ili wapate utaalamu badala ya kuacha kazi hizo zikifanywa na wageni pekee.

Katika hatua nyingine akizungumzia hali ya kukua kwa uchumi hivi sasa nchini, Mtafiti Mwandamizi kutoka REPOA Blandina Kilama anasema pamoja na kuonekana kuwa uchumi wa nchi unakua, lakini bado kasi ya ukuaji wake hairidhishi kwani ni ndogo.

Kilama anasema kwa kawaida, nchi inapokuwa na uchumi mkubwa, kasi yake ya ukuaji inakuwa ndogo, na nchi inayokuwa na uchumi mdogo kasi ya ukuaji wa uchumi wake inakuwa kubwa.

Anasema, wakati uchumi wa Tanzania ukikua kwa asilimia saba, uchumi wa China unakuwa kwa asilimia moja, ikimaanisha kwamba China ina akiba kubwa ya fedha katika mabenki yake kuliko Tanzania.

"Kutokana na kasi ndogo ya kukua kwa uchumi, serikali haina budi kupanga njia sahihi kwa watu wake ili waongeze nguvu zaidi katika sekta ya viwanda,"anasema Kilama.

Aidha, anasema kuwa uchumi wa nchi utaweza kukua kama kutakuwa na bidhaa za kutosha zinazozalishwa ndani lakini pia kama kutakuwa na teknolojia stahiki.

